



# WITO WA MAOMBI YA RUZUKU: DOKEZO LA UTEKELEZAJI WA MIRADI CHINI YA PROGRAMU ZA UTAWALA BORA, USAWA WA KIJINSIA NA UJUMUISHWAJI WA MAKUNDI YA VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU, NA UJENZI WA AMANI.

**MWISHO WA KUPOKEA NI TAREHE 16 JUNI 2022**

## UTANGULIZI.

Foundation for Civil Society (FCS) ni shirika huru la kimaendeleo, la Kitanzania lisilolenga kupata faida, ambalo hutoa ruzuku na huduma za kujengea uwezo Asasi za Kiraia za Tanzania. Tangu kuanzishwa kwake FCS imechangia kwa kiwango kikubwa katika kuimarisha uwezo wa sekta ya kiraia nchini Tanzania. Kwa namna moja ama nyingine imeziwezesha asasi za kiraia kuwa na mchango unaoleta chachu ya maendeleo na wananchi kuwa vichochea muhimu vya kuleta ushawishi chanya wa utawala wa kidemokrasia nchini Tanzania, ili kuboresha uwepo wa utoaji wa huduma bora zaidi, hasa katika ngazi za chini za jamii na hatimaje kuboresha maisha kwa wote.

FCS imepitisha mkakati mpya, Mkakati wa 2022-2026 ambao unataka kuona "Wananchi waliowezeshwa, wastahimilivu na wanaowajibika wanapata haki za kiuchumi, za kijamii na kuboresha ubora wa maisha". Hili litafikiwa kwa "kuchangia maendeleo endelevu na shirikishi nchini Tanzania kwa kuimarisha uwezo, kugawana rasilimali, na ushirikiano wa kimkakati na AZAKi, vikundi vya jamii pamoja na watendaji wengine wa maendeleo. Iwapo utapenda kupata taarifa zaidi kuhusu FCS, tembelea tovuti yetu: [www.thefoundation.or.tz](http://www.thefoundation.or.tz).

## KUHUSU WITO HUU

Wito huu wa maombi ya ruzuku kupitia dokezo la mradi unakaribisha Asasi za Kiraia Tanzania (kutoka Bara na Zanzibar) ambazo zimefanikiwa kujiandikisha katika tovuti ya washirika wa FCS kutekeleza miradi katika maeneo makuu 3 ambayo ni;- i) Usawa wa Jinsia, Watu Wenye Ulemavu & Ushirikishwaji wa Vijana ii) Utawala (SAM/PETS) na iii) Ujenzi wa ya Amani na Mshikamano wa Kijamii.

## Fursa za Ruzuku katika Wito huu Maombi.

Wito huu wa maombi ni kwa aina zote za ruzuku zinazotolewa na FCS. Muda wa utekelezaji wa mradi ni miaka 2. Maelezo ya kina juu ya aina na ukubwa wa ruzuku yamewekwa hapa chini;

### i) Ruzuku ndogo ni kati ya TZS 0 – TZS 50,000,000/=

Ruzuku hii inatoa mwanya kwa mashirika madogo, machanga na mapya yenye mawazo bora ya kutatua changamoto katika maeneo yao kupata ruzuku kutoka FCS. Msaada huu hautanufaisha AZAKi pekee bali pia vikundi vya Jumuiya, watu binafsi na asasi mpya zilizoanzishwa.

### ii) Ruzuku ya Kati: kuanzia 50,000,001 hadi TZS 100,000,000 kwa mwaka 1.

Aina hii ya ruzuku inalenga mashirika ya ukubwa wa kati kwa AZAKi ili kutekeleza miradi kwenye maeneo ya matokeo yaliyoainishwa hapo juu. *Kipindi cha utekelezaji wa mradi kitakuwa ni mwaka mmoja* na yaliyoomba ruzuku katika uwiano ulianishwa hapo juu kwenye wito, na yenye uwezo wa kutekeleza miradi na kusimamia rasilimali fedha kwa ufanisi.

### iii) Ruzuku ya Kimkakati : Kuanzia TZS 100,000,000 Hadi 200,000,000 kwa mwaka 1

Hii ndiyo ruzuku kubwa zaidi (kwa kiwango cha fedha) ambayo FCS inatoa. Ruzuku hii inalenga mitandao mikubwa ya Asasi za Kiraia, mashirika mwamvuli na Asasi za Kiraia zinazofanya kazi katika ngazi ya Kitaifa zenye rekodi nzuri ya usimamizi wa fedha na mafanikio makubwa kwenye ushawishi wa kisera katika ngazi ya kitaifa.

FCS itapanga na kumtaarifu mdau kiwango halisi cha ruzuku atakachopatiwa kulingana na ruzuku zilizopo katika mwaka husika wakati wa uandaji wa miradi na nyaraka muhimu.

Ili kuweza kufikia wito huu kwa taarifa za kina ni lazima shirika liwe limesajili katika tovuti ya washirika wa FCS ambayo inapatikana kwenye kiungo [www.smartgrants.co.tz/partnerportal](http://www.smartgrants.co.tz/partnerportal) Kiungo hiki pia kinaweza kupatikana kupitia tovuti ya FCS [www.thefoundation.or.tz](http://www.thefoundation.or.tz)